**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

Telegram: “MAWASILIANO”
Simu: 255 26 2324513
Nukushi: 255 26 23211027
Barua Pepe: ps@mawasiliano.go.tz
Tovuti: www.mawasiliano.go.tz

Mji wa Serikali,
Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Ujenzi,
S.L.P. 677,
**40470 DODOMA**

**Dodoma**
**29 Januari, 2024**

## TAARIFA KWA UMMA

### KIKAO CHA UFUNGUZI WA UJENZI WA CHUO MAHIRI CHA TEHAMA NA NAFASI ZA UFADHILI WA MAFUNZO YA TEHAMA KWA WATUMISHI WA UMMA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 12 Septemba, 2021 aliunda Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu (Instrument) kupitia tangazo la Serikali Na. 782 la tarehe 22 Novemba, 2021 pamoja na majukumu mengine Wizara imepewa jukumu la kufanya tafiti, maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA pamoja na kuendeleza wataalam wa TEHAMA nchini.

Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatekeleza miradi miwili ya ujenzi wa Vyuo vya TEHAMA katika Jiji la Dodoma eneo la Nala pamoja na eneo la Buhigwe, mkoani Kigoma. Utekelezaji wa miradi hii ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa tatu wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2021/2026 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020/2025 ambayo inasisitiza uwepo wa mafunzo ya Ujuzi na Ubunifu katika TEHAMA nchini. Ujenzi wa vyuo hivi vya TEHAMA vitachochea maendeleo katika wakati huu wa Mapinduzi ya 4, 5, na 6 ya viwanda ambayo ndiyo chachu ya ukuaji wa uchumi wa kidigitali duniani.

Vyuo hivi vya TEHAMA vitakuwa kitovu cha taaluma, ujuzi, ubunifu, tafiti, maarifa na kukuza ujasiriamali wa kidijitali Kitaifa na Kimataifa. Vyuo hivi pia vitaifanya Tanzania kuwa mahali pazuri pa-kuvutia Utalii wa Kidijitali, kujifunzia, na kuongeza uwekezaji kutokana na upatikanaji endelevu wa jamii yenye Maarifa yanayoendana na kasi ya mabadiliko ya Teknolojia duniani.

Tarehe 14 Oktoba, 2021 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati akihutubia katika kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru kwenye Viwanja vya Magufuli, wilayani Chato, Mkoani Geita aliahidi kuwa Serikali itajenga chuo kikubwa cha TEHAMA ambacho kitasaidia kutoa ujuzi kwa vijana wote wanaojishughulisha na TEHAMA.

Katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ilianza maandalizi ya ujenzi wa Chuo Mahiri cha TEHAMA ambacho kinajengwa katika eneo la NALA Jijini Dodoma ambacho kitakuwa kinatoa mafunzo ya ujuzi kwa vijana na wabunifu nchini kuhusu masuala ya TEHAMA, kama vile Teknolojia zinazoibukia (Emerging Technologies), Usalama wa Mifumo ya Mawasiliano pamoja na utengenezaji wa mifumo ya TEHAMA.

Chuo hiki kitakuwa ni tofauti na vyuo vingine kwa kuwa ni chuo ambacho kitakuwa kinatoa mafunzo ya ujuzi kwa muda mfupi kwa njia ya moduli kulingana na mahitaji kwa nyakati husika na baada ya moduli kuisha mhitimu atakuwa amepewa ujuzi kwenye eneo mahususi na kumuwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija, na hii itapelekea vijana wengi kujiajiri kwa haraka au kuajiriwa katika Sekta ya TEHAMA kulingana na mahitaji.

Utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa chuo mahiri eneo la Nala, jijini Dodoma katika hatua za awali, unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha upembuzi yakinifu pamoja na uandaaji wa mitaala na miongozo ya chuo hicho. Fedha zitakazotumika kujenga Chuo hicho ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea kupitia Exim benki ya Korea. Aidha, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imewapata washauri elekezi kutoka (Hanyang University Consortium, Yuil Engineering na Moon Engineering) kwa ajili ya kuanza hatua ya upembuzi yakinifu ambao utachukua miezi sita hadi kukamilika kwake.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inautangazia umma kuwa maandalizi ya Ujenzi wa Chuo Mahiri cha TEHAMA utakaofanyika katika eneo la Nala, Dodoma yameanza rasmi leo tarehe 29 Januari, 2024

Sambamba na hilo, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeweka mpango wa ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa umma mia tano (500) ambapo kwa awamu ya kwanza wanafunzi ishirini (20) wamepata ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu katika vyuo vikuu vya nje ya nchi.

Pia, Wizara imetenga nafasi kwa ajili ya wataalamu arobaini (40) kwenye mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi ambapo kati ya hao 15 ni Maprofesa kutoka Chuo Kikuu cha Dar- es Salaam (5), Chuo Kikuu cha Dodoma (5) pamoja na Mbeya University of Science and Technology (MUST - 5). Nafasi 15 tutazitoa kwa watumishi wa Umma kutoka kwenye Taasisi ya benki ya Tanzania (BOT (5) – block chain), Mamlaka ya Mapato (TRA (5), Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA (5) – na nafasi kumi (10) tutazitoa kwa Watumishi wa Umma kwenda kusoma kwenye masoma ya Anga za Juu (Space Technology).

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Utumishi imetangaza nafasi mia nne arobaini (440) za ufadhili wa ambapo kati ya hizo nafasi 410 ni za muda mfupi na thelathini (30) ni za muda mrefu kwenye masuala ya TEHAMA na Teknolojia zinazoibukiwa kwa watumishi wa umma. Dirisha la maombi ya mafunzo hayo limefunguliwa rasmi kupitia tovuti ya www.scholarships.mawasiliano.go.tz.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali**